# 102 - KISWAHILI

## MADHUMUNI YA UJUMLA

1. Kuendeleza mafunzo ya Kiswahili yaliyoshughulikiwa katika shule za msingi.
2. Kumpa mwanafunzi uwezo wa kudumu wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika ipasavyo kwa lugha ya Kiswahili.
3. Kumwezesha kubuni, kuchambua na kujieleza wazi kimantiki.
4. Kutumia Kiswahili katika mawasiliano na shughuli za kila siku.
5. Kutambua, kudadisi, kuthamini na kustawisha aina na tanzu mbalimbali za lugha na fasihi kwa Kiswahili.
6. Kujifunza na kuthamini fani mbalimbali za tamaduni kwa kutumia Kiswahili.
7. Kuwa na utambuzi kwa mambo yanayohusu na yanayoiathiri jamii k.m. ukimwi, maendeleo ya kiteknolojia, usawa wa kijinsia n.k.
8. Kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kudumisha uhai na kujitimizia mahitaji ya kila siku na ya maisha ya baadaye.
9. Kufurahia kujisomea na kujiendeleza mwenyewe kadiri ya uwezo wake.
10. Kuthamini, kufurahia na kujivunia Kiswahili kama lugha ya taifa na kimataifa.

### 1.1.0 KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

### 1.1.1 Shabaha

Kufikia mwisho wa mafunzo ya Kiswahili katika shule ya upili, mwanafunzi aweze:

a) kuzingatia, kuimarisha na kuendeleza umilisi na uzoefu wa matamshi bora katika lugha ya Kiswahili;
b) kutambua na kurekebisha athari zitokanazo na lugha za mama na lugha nyinginezo;
c) kustawisha mawasiliano yafaayo kulingana na kaida za jamii kutegemea mahusiano, mada na mahitaji ya sajili;
d) kusikiliza, kufahamu na kutekeleza ipasavyo;
e) kubuni na kujieleza kikamilifu na kimantiki;
f) kukuza uwezo wa kukusanya na kuhifadhi kazi za fasihi simulizi
g) kukuza utendaji wa kisanii;
h) kukuza kiwango cha msamiati kwa ajili ya mawasiliano mbalimbali;
i) kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na kuionea fahari;
j) kuzingatia na kuhakiki na kuchanganua kazi mbalimbali za fasihi;
k) kueleza historia na maendeleo ya Kiswahili na kuionea fahari kama lugha ya taifa letu;
l) kuzingatia mafunzo na maadili yanayojitokeza katika kazi mbalimbali kwa Kiswahili;
m) kueleza nafasi ya Kiswahili nchini kama lugha ya taifa na kimataifa.

**1.1.2 Yaliyomo**

**Matamshi bora**

a) Kiimbo
b) Shadda
c) Irabu/vokali - */a/, /e/, /i/, /o/, /u/.*
d) Konsonanti - */b/, /ch/, /d/, /dh/, /f/, /g/, /gh/, /h/, / j/, /k/, /l/, /m/, /n/, /ng'/, /ny/, /p/, /r/, /s/, /sh/, /t/, /th/, /v/, /w/, /y/, /z/.*
e) Ala za sauti/kutamkia
f) Namna ya kutamka na aina za sauti k.m. ghuna, sighuna/hafifu, vipasuo, vikwamizo n.k.
g) (i) silabi si-la-bi
   (ii) silabi tatanishi
h) Maneno
i) Vitate k.m. baba, papa
j) Vitanza ndimi

**Maamkizi na mazungumzo**

a) Maamkizi na mazungumzo katika muktadha mbalimbali – nyumbani, dukani, mtaani, sokoni, shuleni, hotelini, hospitalini, posta, kituo cha polisi, mahakamani n.k
b) mahojiano
c) mijadala
d) hotuba

**Ufahamu wa kusikiliza:** Ufahamu wa taarifa za kusikiliza

**Kusikiliza na kudadisi**

a) Dhima ya fasihi kwa jumla – (i) Maana na (ii) Aina
b) Fasihi simulizi: Vipera vya fasihi simulizi

   i) Hadithi : utambaji na masimulizi – hurafa, hekaya, Visasili, Mighani, Ngano, na miviga.
   ii) Semi: Methali, Vitendawili, mafumbo na chemsha bongo, Misemo, Lakabu, Misimu, na Tanakali za sauti
   iii) Ushairi - Nyimbo
   iv) Ngomezi – fasihi ya ngoma kuhusu ujumbe

c) Maigizo

**2.1.0 SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

**2.1.1 Shabaha**

Kufikia mwisho wa mafunzo ya kiswahili katika shule ya upili mwanafunzi aweze:

a) kubainisha maana na dhima ya lugha;
b) kueleza misingi ya uainishaji wa maneno ya Kiswahili;
c) kukuza uwezo wa kutumia sauti, maneno ya Kiswahili sanifu katika mawasiliano ya kimazungumzo na kimaandishi;
d) kutambua na kurekebisha makosa ya kisarufi na matumizi ya lugha/kimantiki;

e) kukuza uwezo wa kutumia msamiati na istilahi;
f) Kufafanua maana na aina za tungo;
g) Kuchanganua sentensi na kufafanua maana, aina na vijenzi vya sentensi.

### 2.1.2 Yaliyomo

1. **Lugha**
   a) Maana na dhima ya lugha
   b) Sauti: Irabu/vokali, Konsonanti, Mpangilio wa sauti katika silabi na maneno
   c) Vipashio vya lugha: sauti-silabi-neno- sentensi

2. **Misingi ya maneno**
   a) Mofimu: i) Maana na ii) Aina
   - Huru
   - Tegemezi

   b) Viambishi – i) maana na ii) aina
   - Awali
   - Tamati

3. **Aina za maneno na migawanyiko yake:** Aina za maneno
   a) ***Nomino* N -** jumla/kawaida, pekee, dhania, kitenzi jina, jamii, na nomino za wingi.

   b) ***Vivumishi* V** – sifa, , vionyeshi, vimilikishi, viulizi, idadi, pekee, majina, unganifu, virejeshi, na visisitizi

   c) ***Vitenzi* T -** vitenzi halisi, vitenzi vikuu, visaidizi, vishirikishi vipungufu, vishirikishi vikamilifu, na vitenzi sambamba

   d) ***Viwakilishi* N** – vionyeshi, vimilikishi, viulizi, virejeshi, ‘A’ unganifu, sifa, nafsi, ngeli, pekee, idadi, visisitizi, na ‘O’ rejeshi

   e) **Vielezi E - Vielezi vya:**
   i) Namna/jinsi – vikariri, halisi, mfanano, hali, ala/vitumizi, na viigizi.
   ii) Wakati – viambishi na idadi/jumla
   iii) Idadi/Kiasi - idadi halisi na maneno kamili
   iv) Mahali – viambishi na maneno kamili

   f) **Viunganishi U**
   g) **Vihusishi H**
   h) **Vihisishi I**

4. **Ngeli za nomino -** A – WA, U – I, U – YA, YA – YA, LI – YA, KI – VI, I – ZI, I - I, U – ZI, U – U, KU -, PA-KU-MU.
5. **Umoja na wingi**
   Ngeli za nomino k.m. A-WA

U-I, LI-YA n.k. na upatanisho wa kisarufi kwa mintaarafu ya viambishi:
a) Awali vya vitenzi
b) Vya vivumishi vya sifa
c) Vya vivumishi vya pekee – enye, -enyewe, -ingine, -ote, -o-ote, -ingineo

6. **Misingi ya maneno**
   a) Mofimu - i) Maana na ii) Aina
      - Huru
      - Tegemezi
   b) Viambishi – i) Maana na ii) (ii) Aina
      - Awali
      - Tamati

7. **Matumizi ya maneno na viambishi maalumu**
   a) Viambishi: -ku-, -ndi-, -ji-

   b) Maneno: Jinsi, Namna, Ila, Japo, Ijapokuwa, Ingawa, Ingawaje, Ikiwa, Wala, Walakini, Kwa, Labda, Na

8. **Nyakati na hali**
   a) Nyakati: LI, NA, TA
   b) Hali: ME, HU, NGE, NGELI, NGALI, A, KA, KI, KU
   c) Hali ya kuamuru
   d) Ukanushaji kutegemea nafsi na: i) Nyakati, ii) Hali

      i) Nyakati
         - Uliopita -LI-
         - Uliopo -NA-
         - Ujao - TA-
      ii) Hali
         - Hali timilifu -ME-
         - Hali ya mazoea -HU-
      iii) Ukanushaji kutegemea nafsi na:
         - Nyakati - LI-, -NA-, -TA-
         - Hali -ME-HU-

9. **Mnyambuliko wa vitenzi**
   a) Kauli za vitenzi – Kutendwa, Kutendewa, Kutendeka, Kutendana, Kutendeana, Kutendeshwa, Kutendeshana, Kutendeshea, Kutenda, Kutendesha
   b) Mnyambuliko wa vitenzi vya: Asili ya kigeni, , Silabi moja, Asili ya kibantu,
   c) Kauli za vitenzi vya kibantu: Kutendeshewa, Kutendesheana, Kutendesheka, Kutendama, Kutendata, Kutendua, Kutenduka
   d) Mnyambuliko wa vitenzi vya silabi moja katika kauli mbalimbali: ja, nywa, nya, pa, fa, la, cha, pwa, chwa, wa
   e) Mnyambuliko wa vitenzi vyenye asili ya kigeni k.m. samehe, ghairi, tubu, n.k. katika kauli mbalimbali.

10. **Sentensi ya Kiswahili**

a) Maana ya sentensi
b) Mpangilio na uhusiano wa maneno kimantiki katika sentensi ya Kiswahili.

11. **Sentensi ya Kiswahili**

a) Aina za:
   i) Virai: vihusishi, nomino, vivumishi, na vielezi.
   ii) Vishazi: huru na tegemezi
b) Muundo wa sentensi
   i) Miundo ya kikundi/nomino (KN)
   ii) Miundo ya kikundi/tenzi (KT)
   iii) Yambwa/shamirisho (SH): kipozi, kitondo, ala/kitumizi
   iv) Chagizo (CH)

c) Aina za sentensi: i) Sahili, Ambatano, Changamano

d) Uchanganuzi/upambanuzi wa aina mbalimbali za sentensi kwa njia ya

e) Jedwali,Mchoro wa matawi, Mstari

12. **Uakifishaji**

Matumizi sahihi ya alama za kuakifisha:

Nukta/kitone/kikomo (.), Mkato/kitone/kipumuo/kituo/koma (,), Nukta mkato/semi koloni (;), Nukta pacha/nukta mbili/koloni (:), Kiulizi/kiulizo (?), Alama hisi (!), alama mtajo/za kunukuu/za usemi (" "), Mkwaju/mshazari (/), Kistari kifupi (-), Kistari kirefu ( - ), Mstari (_______), Ritifaa/kibainishi ('), Mabano/vifungo/Parandesi ( ), Herufi kubwa (H) na herufi ndogo (h), Herufi nzito **(Hh),** Herufi mlazo/italiki *(Hh),* Nukta za dukuduku/mdokezo (…), Kinyota (*)

13. **Uakifishaji:** Uakifishaji wa maandishi ya aina mbalimbali k. m. sentensi, aya, vifungu n.k.

14. **Usemi halisi na usemi wa taarifa**

a) Usemi halisi
b) Usemi wa taarifa

## 3.0.0 KUSOMA

### 3.1.0 Shabaha

Kufikia mwisho wa mafunzo ya Kiswahili katika shule ya upili mwanafunzi aweze:

a) kusoma kwa sauti na kuzingatia matamshi bora;
b) kusoma kimya na kubainisha mawazo makuu pamoja na matumizi ya lugha;
c) kuimarisha kusoma kwa kasi;
d) kufahamu na kujibu maswali kwa usahihi na kutekeleza ipasavyo;
e) kukuza uwezo wa kutumia maktaba;
f) kutumia kamusi ipasavyo;

g) kukuza dafina ya msamiati na muktadha na kaida za jamii;
h) kubainisha maadili na mafunzo yanayotokana na maandishi kwa Kiswahili;
i) kusoma kwa kina na kuchambua maandishi kwa Kiswahili;
j) kustawisha umilisi wa matumizi ya msamiati kutegemea muktadha na kaida za jamii;
k) kuelezea historia na chimbuko la Kiswahili na kuonea fahari kama lugha ya taifa letu;
l) kuzingatia maadili na mafunzo yanayojitokeza katika maandishi kwa Kiswahili;
m) kuelezea hali ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru na kuionea fahari kama lugha ya taifa na kimataifa;
n) kufahamu, kujibu maswali kwa usahihi na ipasavyo.

### 3.2.0 Yaliyomo

### 3.2.1 Kusoma kwa sauti na kwa ufa

a) Sauti mwambatano k.m. */mw/, /kw/, /mb/, /ng/, /nj/, /nd/, n.k*
b) Sauti na maneno tatanishi k.m.p/b, s/sh, l/r, ch/sh, s/z (papa/baba, tata/dada. Susu/zuzu
c) Vitate k.m. kua/kuwa, pua,bua, vua/fua
d) Maneno tatanishi yenye sauti mwambatano k.m. mbalimbali, kindani/kidani, buni/mbuni
e) Sentensi zenye maana tatanishi
f) Vitanza ndimi
g) Vifungu vya maneno na aya

### 3.2.2 Kusoma kwa kina

a) Kusoma vitabu viteule: Riwaya, Tamthilia, Ushairi: Mashairi ya arudhi na Mashairi huru, Hadithi fupi

b) Historia na maendeleo ya Kiswahili
   i) Lugha ya Kiswahili baada ya uhuru nchini Kenya
   ii) Wajibu wa Kiswahili kitaifa na kimataifa
   iii) Matatizo yanayoikumba lugha ya Kiswahili
   iv) Mikakati inayofaa kuimarisha lugha ya Kiswahili

**3.2.3 Kusoma kwa mapana:** Kusoma vitabu vya ziada, Magazeti, Majarida, Makala ya runinga na redio, Makala mbalimbali ya kitaaluma kwa kuzingatia uchambuzi wa maswala ibuka kama vile afya na ukimwi, utandawazi na mawasiliano.

**3.2.4 Matumizi ya maktaba:** Maana, umuhimu na matumizi ya maktaba

**3.2.5 Matumizi ya kamusi;** Maana, aina, umuhimu na matumizi ya kamusi k.m. kamusi ya visawe, teknolojia n.k.

## 4.0.0 KUANDIKA

### 4.1.0 Shabaha

Kufikia mwisho wa mafunzo ya Kiswahili katika shule ya upili mwanafunzi aweze:

a) kuandika hati nadhifu zinazosomeka;
b) kuzingatia tahajia sahihi katika maandishi;
c) kuandika miundo sahihi ya sentensi;
d) kuakifisha maandishi ipasavyo;
e) kuandika maandishi yenye mtiririko wa mawazo;
f) kubuni na kuandika kwa kuzingatia kanuni mbalimbali za utungaji;
g) kuandika mikusanyo ya fasihi simulizi ili kuihifadhi.

### 4.2.0 Yaliyomo

4.2.1 **Uandishi wa kawaida:** Majibu ya ufahamu, mukhtasari, imla na uchambuzi/uhakiki wa maandishi mbalimbali

4.2.2 **Utungaji wa kiuamilifu:**

Barua (kirafiki, rasmi, memo, simu, kwa mhariri, meme -nukulishi, mdahilishi, ujumbe wa rununu/simu-tamba), Hotuba, Ratiba k.m. tamasha za michezo ya kuigiza, Matangazo, Maagizo/maelezo, Tahadhari (ilani, na onyo), Tawasifu, Shajara, Kumbukumbu, Mahojiano na dayolojia, Insha za kitaaluma k.m. makala ya redio na runinga, Resipe, Orodha ya mambo, Taarifa, Hojaji, Kujaza fomu, stakabadhi na orodha, Risala

**4.2.3 Uandishi wa Insha:** Methali, Masimulizi, Mazungumzo, Mawazo, Maelezo, Mdokezo

**4.2.4 Utungaji wa kisanii**

a) Mashairi:i) Mashairi ya arudhi, ii) Mashairi huru
b) Mikusanyo ya kazi za kisanii
c) Vitendawili, mafumbo na chemsha bongo
d) Vitanza ndimi
e) Michezo ya kuigiz
f) Tahakiki za kazi za kisanii.

**4.2.5 Uakifishaji**

a) Kuakifisha maandishi ya aina mbalimbali
b) Usemi halisi
c) Usemi wa taarifa.

**4.2.6 Uundaji wa maneno**

a) Nomino kutokana na mzizi wa nomino
b) Nomino kutokana na mzizi wa kitenzi
c) Kitenzi kutokana na mzizi wa nomino
d) Kivumishi kutokana na mzizi wa nomino
e) Nomino kutokana na mzizi wa kivumishi
f) Kivumishi kutokana na mzizi wa kitenzi

g) Kitenzi kutokana na mzizi wa kivumishi

### 4.2.7 Uundaji wa nomino

Nomino kutokana na vitenzi vya asili ya kigeni